



## RIPOTI YA WARSHA YA KUELIMISHA UMMA KUHUSU UWAZI NA UWAJIBIKAJI KATIKA SEKTA ZA MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA

**Tarehe:** 02 Februari 2026

**Mahali:** Ukumbi wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Mkoawa Mtwara

**Mratibu:** Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)

---

### 1. UTANGULIZI

Taasisi ya TEITI iliandaa warsha ya kuelimisha umma kuhusu shughuli za uwazi na uwajibikaji katika sekta za madini, mafuta na gesi asilia, iliyofanyika tarehe 02 Februari 2026 katika Ukumbi wa BOT, Mkoa wa Mtwara Warsha ilifunguliwa rasmi na Katibu Mtendaji wa TEITI ambaye aliwakaribisha wageni waalikwa na washiriki wote, pamoja na kumshukuru mgeni rasmi kwa kuhudhuria. Katika hotuba yake ya ufunguzi, alieleza kwa ufupi historia ya TEITI kama taasisi iliyoanzishwa chini ya mwamvuli wa EITI, pamoja na majukumu yake katika kusimamia uwazi na uwajibikaji katika sekta ya uziduaji.

---

### 2. MALENGO YA WARSHA

Warsha ilikuwa na malengo yafuatayo:

1. Kuwajengea wananchi na wadau uelewa kuhusu manufaa ya kodi na mapato yanayotokana na makampuni ya uziduaji.
  2. Kutoa elimu kuhusu umuhimu wa uwazi, ushirikishwaji na uwajibikaji wa makampuni kwa wananchi.
  3. Kuwahamasisha wananchi na wadau kuhoji na kufuatilia mafanikio yatokeanayo na mapato ya sekta ya madini, mafuta na gesi asilia.
  4. Kuelimisha umma kuhusu mchakato wa ulinganishwaji wa mapato yanayotolewa na makampuni na yanayopokelewa na Serikali.
-

### **3. WASHIRIKI WA WARSHA**

Warsha ilihudhuriwa na washiriki zaidi ya 150 kutoka Mikoa ya Lindi na Mtwara

Washiriki walijumuisha:

- Wanafunzi na wahadhiri kutoka Chuo cha SAUTI
  - Madiwani na wenye viti wa mitaa
  - Watumishi wa Halmashauri na Manispaa za Lindi na Mtwara
  - Wadau wa sekta ya uziduaji
  - Wawakilishi wa Asasi za Kiraia
- 

### **4. MADA ZILIZOWASILISHWA**

Warsha ilijadili mada zifuatazo:

#### **4.1 TEITI na MajukumuYake**

Mtoa mada kutoka TEITI alieleza muundo wa taasisi hiyo unaosimamiwa na Kamati ya Multistakeholder Group (MSG) yenye wajumbe nane kutoka Serikalini, Makampuni ya Uziduaji na Asasi za Kiraia. Alifafanua pia kuhusu mchakato wa uteuzi wa Mwenyekiti wa Kamati na jukumu la TEITI katika kuandaa na kuchapisha taarifa za Uwazi wa Mapato.

#### **4.2 Asasi ya Kiraia – Hakirasilimali**

Mwakilishi wa Hakirasilimali alieleza kuwa taasisi hiyo ni mwamvuli wa Asasi za Kiraia unaojikusha na uchambuzi na tafiti katika Sekta ya Uziduaji Alisisitiza jukumu lao la kushauri kuhusu sera, sheria na matumizi ya mapato ili kuhakikisha rasilimali zina wanufaisha wananchi, pamoja na kufuatilia mianya ya rushwa na mikataba isiyonatija.

#### **4.3 Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC)**

Mtoa mada kutoka NEMC alieleza majukumu ya Baraza hilo katika kufanya ukaguzi na kupitisha tathmini za athari za mazingira kabla ya kuanza kwa shughuli za utafiti na uchimbaji. Aidha, alieleza wajibu wa NEMC katika kulinda mazingira, kuimarisha uelewa wa jamii, na kushirikiana na Serikali za mitaa katika kushughulikia masuala ya uharibifu wa mazingira.

---

### **5. NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA MAFUNZO**

Mafunzo yaliendeshwa kwa njia zifuatazo:

### **(a) Mihadhara**

Wawakilishi wa makampuni walieleza juhudi zao za ushirikishwaji wa jamii. Kwa mfano, ilielezwa kuwa kampuni ya Dangote imeajiri zaidi ya asilimia 98 ya wananchi wa ndani. Aidha, makampuni ya gesi asilia yameanzisha program za kusomesha wanafunzi wa vyuo na sekondari katika maeneo husika.

### **(b) Maswali na Majibu**

Washiriki waliuliza maswali mbalimbali kuhusu:

- Fursa za ajira kwa vijana katika sekta ya gesi asilia.
  - Sababu za kupandana kushuka kwa mapato ya Serikali.
  - Migogoro ya mapato ya Service Levy kati ya Halmashauri.
  - Ucheleweshaji wa miradi ya maendeleo kama Shule ya Nanyumbu.
  - Changamoto za wachimbaji wadogo wa chumvi.
- 

## **6. MATOKEO YA WARSHA**

Warsha iliongeza uelewa wa washiriki kuhusu:

- Manufaa ya Sekta ya Uziduaji katika uchumi wa Taifa.
- Mchakato wa uwazi wa mapato.
- Wajibu wa taasisi mbalimbali katika kusimamia Sekta hiyo.

Washiriki walionesha ushiriki mzuri kupitia maswali na michango yenye tija.

---

## **7. CHANGAMOTO ZILIZOJITokeza**

Changamoto kubwa iliyojitokeza ilikuwa ni uhaba wa muda, kutokana na wingi wa mada na maswali ya washiriki.

---

## **8. MAPENDEKEZO**

1. Warsha zijazo zitengewe muda wa kutosha.
  2. Ushiriki wa wadau uongezwe zaidi.
  3. Elimu iendelee kutolewa katika ngazi za jamii zinazozunguka miradi ya Uziduaji.
-

## 9. HITIMISHO

Kwa ujumla, warsha ilifanikiwa na ilitimiza malengo yake kwa kiwango kikubwa. Ushirikiano kati ya TEITI, Taasisi za Serikali, makampuni na Asasi za Kiraia umeonesha umuhimu wa Kuendeleza juhudi za kuimarisha Uwazi na Uwajibikaji katika Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia kwa manufaa ya Taifa.

### Matukio Picha:







